

HATUA ZA UOMBAJI E-PASSPORT

- *Kabla ya kujaza Fomu Mwombaji ahakikishe amefanya scanning ya picha yake (passport size) na viambatisho vyote ambavyo ni: Cheti cha kuzaliwa, cheti cha kuzaliwa ama hati ya kiapo (affidavit) ya mzazi mmoja wapo (Baba au Mama); nakala ya passport na nakala ya kitambulisho chochote cha mwombaji (cha Marekani ama cha Tanzania). Viambatisho hivyo viwe kwenye mfumo wa picha (image- jpeg,jng) na kila kiambatishi kisizidi ukubwa wa 1MB. Viambatisho hivyo atatakiwa kuviupload wakati anajaza fomu*
-
- *Awe na kadi yake ya bank ambayo atatumia kufanya malipo wakati wa kujaza fomu hiyo*
-
- *Kwa Waombaji walio miji ya mbali lazima watume bahasha ama shipping label kwa ajili ya kutumiwa passport zao mara wanapojulishwa kuwa zimepokelewa Ubalozini.*

1. Mwombaji ajaze fomu online kupitia www.immigration.go.tz (e-services) ataona sehemu ya passport application form na awe tayari kulipia ada ya awali ya kiasi cha dola za kimarekani 90;
2. Apakue fomu yake na kuituma kwa mail, au email (ubalozi@tanzaniaembassy-us.org); Fomu hiyo iwasilishwe pamoja na viambatisho vyote vilivyotajwa hapo juu kwenye maelezo ya awali;

3. Ikishapokelewa na kuthibitishwa kwenye mfumo mwombaji atajulishwa achague tarehe za kuja kwa ajili ya finger prints na picha. Taarifa hiyo ataipata kupitia email address aliyojaza kwenye fomu;
4. Kwa wale ambao wana fomu za zamani walizolipia dola 15 watatumiwa Bill kwa ajili ya kukamilisha malipo ya kiasi cha dola 75 kilichobakia. Bill hiyo ya malipo itamwonyesha link ya kufanya malipo kwa njia ya mtandao <https://epay.gepg.go.tz>;
5. Wakati Mwombaji anakuja Ubalozini ahakikishe anakuja na nakala halisi za viambatisho vyake na atapatiwa risiti yake ya malipo; na
6. Passport ikipokelewa kutoka Uhamiaji Mhusika atatumiwa ujumbe kujulishwa ili aweze kukamilisha hatua za kutumiwa passport yake kwa njia ya mail ama kwa kuchukua mwenyewe Ubalozini.

UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Aprili, 2021